

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA TATU

27 APRILI, 2017



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA TATU – TAREHE 27 APRILI, 2017

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

III. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**105. MHESHIMIWA JOHN PETER KADUTU
(ULYANKULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kampuni binafsi za migodi zimekuwa zikikiuka mikataba ya kazi na pia zikikandamiza na kuwanyanya wafanyakazi:-

(a) Je, ni lini Serikali itafanya ukaguzi wa mikataba kwa kampuni zinazofanya kazi migodini;


(b) Je, kwa nini Serikali isiamue kuwaondoa nchini waajiri wakorofi kwa unyanyasaji wanaoufanya.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

106. MHESHIMIWA OTHMAN OMAR HAJI (GANDO)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Moja kati ya kazi za Polisi ni ulinzi na usalama wa raia na mali zao, uzoefu unaonyesha kila zinapotokea Kampeni za Uchaguzi Jeshi la Polisi hutumika kama Taasisi ya Chama Tawala hivyo husababisha ulinzi na usalama (hasa Wapinzani) kutoweka mikononi mwa Polisi:-

Je, Serikali haioni kwamba inalitumia Jeshi la Polisi kwa lengo la kudhoofisha upinzani na kurahisisha kukipatia ushindi Chama chake cha CCM.



107. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (TARIME MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa leseni za udereva katika Mkoa wa Polisi Tarime/Rorya kutokana na kutokuwepo kwa huduma hiyo. Hali hiyo inapelekea Wananchi kupata adha kubwa ya kufuata huduma za leseni Musoma Mjini ambao ni Mkoa mwingine wa Polisi; kutokana na adha hiyo Wananchi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali waliamua

kujenga na kukamilisha jengo la Usalama Barabarani:-

- (a) Je, ni lini Mkoa wa Polisi Tarime/Rorya utafungiwa mitambo ya kutoa leseni za udereva ili kuondoa usumbufu uliopo sasa wa kutumia gharama na muda kwa kufuata huduma hiyo Musoma Mjini;
- (b) Je, ni lini Ofisi za Mkoa wa Polisi Tarime/ Rorya zitajengwa ili kurahisisha utoaji huduma kwa Wananchi.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

108. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Majanga ni mambo yasiyotarajiwa ila huwa yanatokea tu, majanga kama ajali za Baharini Ziwani, barabarani, matetemeko, vimbunga, majanga ya njaa n.k yamekuwa yakitokea:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha na kuimarisha nyenzo na ujuzi kwa Kikosi cha Uokoaji wa Majini kinachojulikana kama “Coast Guard” kwa ajili ya uokoaji.

**109. MHESHIMIWA GODFREY WILLIAM MGIMWA
(KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Tatizo la mawasiliano ya simu katika Jimbo la Kalenga bado ni kubwa:-

Je, ni lini Serikali itapeleka minara ya simu kwenye vijiji vya Kaning'ombe, Ikungwe, Lyamgungwe, Igunda na Ikuvilo.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**DODOMA
27 APRILI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**